

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**



**TAARIFA KWA UMMA**

**MAZINGIRA BORA YA MIRADI KUIPATIA MIKOPO SEKTA BINAFSI TOKA  
KATIKA MASHIRIKA YA KIMATAIFA**

Mazingira bora yakutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika Sekta Binafsi kutaiwezesha sekta hiyo kupata fedha katika Mashirika ya Kimataifa ambayo yametenga bajeti kwa ajili ya kuimarisha sekta hiyo.

Hayo yameelezwa mjini Bali Indonesia na Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Philip Isdor Mpango, baada ya kumalizika kwa mikutano ya mwaka ya Benki ya Dunia (WB) na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) iliyowakutanisha Mawaziri wa Fedha na Magavana wa Benki Kuu wa nchi mbalimbali.

Dkt. Mpango alisema kuwa, yapo Mashirika ambayo yapotayari kutoa fedha iwapo kuna uhakika wakurudishwa kwa fedha hizo kama zitatolewa kwa mfumo wa mikopo, hivyo ni vizuri mazingira ya utekelezaji miradi ya Sekta Binafsi yakaboreshwa ili kuwe na urahisi wa upatikanaji wa fedha hizo.

Alisema kuwa, nchi za Afrika ikiwemo Tanzania zinahitaji pia fedha za kuwekeza kwenye miundombinu ya kiteknolojia ili kuweza kuchochea ukuaji wa uchumi

“Kama nchi inatakiwa kuhakikisha inaongeza mapato ya ndani ya kodi na yasiyo ya kodi kwa kuwa jambo hilo ni moja ya kigezo chakuweza kupata fedha zaidi kutoka Mashirika ya Kimataifa”, alieleza Dkt. Mpango.

Naye Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dkt. Yamungu Kayandabila, alisema kuwa katika mikutano ya mwaka ya WB na IMF, imesitiza kuondoa vikwazo vya kibiashara kati ya nchi na nchi kwa kuwa biashara inamchango mkubwa katika kukuza pato na uchumi wa nchi ambapo unategemea mahusiano mazuri kati ya taifa moja na lingine.

Dkt. Kayandabila alisema kuwa, Mataifa makubwa ikiwemo China na Marekani yanatakiwa kupunguza mvutano unaosababishwa na vikwazo vya kodi baina yao ili kutoathiri nchi ndogo ikiwemo Tanzania inayofanya biashara na nchi hizo.

Mikutano ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa imemalizika mjini Bali Indonesia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa IMF, Bi. Christine Lagarde na Rais wa Benki ya Dunia Bw. Jim Yong Kim, kukutana na Mawaziri wa Fedha na Magavana wa Benki Kuu ambapo waliangazia mwenendo wa uchumi wa ulimwengu hasa Afrika ambayo uchumi wa baadhi ya nchi unaenda vizuri na nyingine kutofanya vizuri na kusababisha Bara hilo kuonekana uchumi wake kukua kwa kasi ndogo.

**Imetolewa na:**

**Kitengo cha Habari na Mawasiliano  
Wizara ya Fedha na Mipango  
Bali Indonesia**